

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS,
Idara Kuu ya Utumishi,
S.L.P. 2483
DAR ES SALAAM.
24 Desemba, 1992.**

Kumb. Na. MUF.3/33/635/90

WARAKA WA UTUMISHI NA. 9 WA MWAKA 1992

**UTARATIBU WA KUAJIRI NA KUTUMIA VIZURI WATAALAM
WAZALENDO NJE NA NDANI YA UTUMISHI WA SERIKALI**

UTANGULIZI:

Waraka wa Utumishi Na. 4 wa mwaka 1991 uliweka utaratibu wa kuajiri na kuwatumia Wataalam Wazalendo katika miradi, mipango na huduma nyingine ambazo huendeshwa na Mashirika ya Kimataifa na Wahisani wa Nchi za Nje. Utaratibu huo sasa unafanyiwa marekebisho ili kuondoa utatanishi wa tafsiri wa baadhi ya vipengele vya Waraka huo, hasa katika masuala ya malipo ya mshahara, masharti ya kazi na suala la malipo ya izeeni (Pension).

**MASHIRIKA YA UMOJA WA MATAIFA NA MASHIRIKA
MENGINE YA KIMATAIFA:**

2. Ajira ya Watanzania katika Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ambayo Tanzania ni mwanachama ni jambo linalokubaliwa na kuungwa mkuoni na Serikali. Mbali ya kuwa ni moja ya maeneo ya kuwapatia kazi wananchi wetu, ajira katika mashirika hayo zinatoa nafasi ya kuongeza upeo, ujuzi na uzoefu na hivyo kuwaendeleza wataalam hao kwa manufaa yao wenye, ya Mashirika hayo na vilevile kwa manufaa ya Taifa. Watanzania wanaoajiriwa na Mashirika ya Kimataifa wanatazamiwa kuwa wawakilishi wa Taifa katika mashirika hayo. Aidha, mishahara na marupurupu mengine wanayolipwa huko yanachangia katika kukua kwa pato la Taifa hususan kutunisha mfuko wa fedha za kigeni.

3. Kwa hiyo Wataalam' Wazalendo walio katika utumishi wa Serikali ambao wataajiriwa kwenye Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ambayo Tanzania ni mwanachama kwa kupewa nafasi hizo na Serikali au kwa kujitafutia ajira hizo kwa nija zao wenye, wataajiriwa Juu la Banda ya Kujitafutia Ajira nafasi wa aya ya aina ya Waraka huu. Wataalazimka kuomba likizo bila malipo kwa kipindi chote cha ajira katika Mashirika hayo na kuzingatia masharti yaliyomo kwenye Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 5 wa mwaka 1986 kuhusu Likizo Bila Malipo.

MIRADI YA SERIKALI INAYOENDESHWA KWA USHIRIKIANO NA WAFAÐHILI:

4. Wataalam Wazalendo walio katika utumishi wa Serikali ambao watatakiwa kufanya kazi kwenye miradi ya Serikali inayosaidiwa na Wafadhili, watakubaliwa kufanya kazi huko kwa utaratibu wa kushikizwa (attachment) kwa muda wote watakaohitajika huko bila kuathiri masharti ya ajira zao Serikalini. Ushikizwaji utazingatia masharti muhimu yafuatayo:—

- (a) Miradi itakayokubaliwa kutekelezwa na Wataalam wa kushikizwa ni ile inayoendeshwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wafadhili.
- (b) Wataalam watakaohesabika kuwa wako kwenye mradi kwa kushikizwa watakuwa wale ambao nafasi watakazojaza zitakuwa zimekubaliwa chini ya mkataba wa kulipwa kwa fedha za mradi.
- (c) Utaratibu wa kushikiza hautaathiri masharti ya ajira Serikalini na malipo ya Uzeeni ya Wataalam watakaoshikizwa.
- (d) Mtaalam ataendelea kulipwa mshahara wake na Serikali. Pia atalipwa tofauti kati ya mshahara wake na ule wa mradi kama posho ya ziada (Topping Up Allowance).

5. Ili kuondoa utatanishi, pale aibapo masharti ya mkataba wa kushikizwa kwenye mradi ni pamoja na kulipwa kiinua mgongo (gratuity) kwa kipindi hicho cha kushikizwa basi mtaalam anayehusika atahesabika kama yuko katika Likizo Bila Malipo. Hivyo hatalipwa mshahara na Serikali kwa kipindi hicho na muda huo hautahesabika katika hesabu za malipo ya Pensheni.

MIRADI INAYOENDESHWA NA WAFANYAKAZI:

6. Wataalam Wazalendo watakaoajiriwa katika miradi ya hapa nchini inayoendeshwa na kugharamiwa na wafadhili peke yao watakuwa huko laje ushishabu wa Likizo Bila Malipo na wataalipwa mshahara na Wataalam wile yeye miradi.

UTARATIBU WA KUCHUKUA "SABBATICAL LEAVE":

7. Serikali ilikwishakubali watumishi wake kuruhusiwa kuchukua "Sabbatical Leave" tangu mwaka 1980 katika mpango wa Mafunzo ya "Top Executives". Utaratibu huu utatumika kwa kazi zinazoongeza uzoefu na ujuzi kwa Mtaalam katika fani yake. Hivyo "Sabbatical Leave" itatolewa chini ya masharti yafuatayo:—

- (a) Mtaalam atakayestahili kupewa "Sabbatical Leave" ni yule mwenye mshahara wa ngazi ya GS. 10/RP. 7 na kuendelea juu.
- (b) Muda wa "Sabbatical Leave" hautazidi miezi kumi na mbili (12) na itatolewa mara moja tu katika mzunguko wa miaka mitano.
- (c) Mtaalam aliye katika "Sabbatical Leave" ataendelea kulipwa mshahara wa Serikali ila hatapata maslahi mengine kama vile likizo ya kawaida kwa kipindi hicho chote.

MWISHO:

8. Idhini ya kuruhusu ajira za Wataalam Wazalendo kwa utaratibu wa Likizo Bila Malipo au Kushikizwa na idhini ya kuchukua "Sabbatical Leave" kwa mujibu wa Waraka huu itaendelea kutolewa na Katibu Mkuu (Utumishi).

9. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Januari, 1993 na unafuta Waraka wa Utumishi Na. 4 wa mwaka 1991.

D. A. NTUKAMAZINA,
Katibu Mkuu (Utumishi)